

HALI YA UTUMISHI NA UTAWALA BORA

Maeneo ya Kiutawala

Wilaya ina Tarafa 2 Kata 18, Vijiji 71, na Vitongoji 317. Wilaya ina jumla ya madiwani 24, ambapo Madiwani wa kuchaguliwa ni 18 na viti maalum (6), madiwani wote wanatoka chama cha Mapinduzi (CCM). Aidha Wilaya ina jimbo 1La uchaguzi na Mbunge 1 wa kuchaguliwa kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM). Kwa mujibu wa muundo mpya wa kiutumishi Halmashauri ina Divisheni 9 na vitengo 9. Idara zenye Wakuu wa Divishen na Vitengo wenye uteuzi rasmi ni 7 Wilaya ya Ileje ina jumla ya Watumishi 1,388 kati ya Watumishi 2,620 wanaohitajika hivyo kuna upungufu wa watumishi 1,178 (45.%) kama inavyooneshwa kwenye jedwali hapo chini;

Jedwali 1: Hali ya Watumishi Halmashauri ya Wilaya ya Ileje

Na	IDARA	MAHITAJI	WALIOPO	UPUNGUFU
1.	Utawala na usimamizi wa Rasilimali watu	240	114	125
2.	Viwanda, Biashara na Uwekezaji	10	4	6
3.	Idara ya Mipango na uratibu	6	4	2
4.	Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe	648	304	344
5.	Miundombinu, vijijini na Mijini	30	19	11
6.	Kilimo, Mifugo na Uvuvi	157	39	118
7.	Elimu ya Awali na Msingi	1005	568	437
8.	Elimu Sekondari	433	314	66
9.	Maendeleo ya Jamii	23	10	13
	Jumla ndogo	2585	1374	1157
	VITENGO	MAHITAJI	WALIOPO	UPUNGUFU
1.	Huduma za Sheria	4	0	4
2.	Ukaguzi wa Ndani	5	2	3
3.	Usimamizi wa ununuzi	7	3	4
4.	Tehama	5	1	4
5.	Fedha na Uhasibu	14	8	6
6.	Michezo, Utamaduni na Sanaa	2	2	0
7.	Mawasiliano Serikalini	2	0	2
8.	Usimamizi wa Taka na Usafi wa mazingira	3	1	2
9.	Uhifadhi wa Maliasili na Mazingira	10	3	7
	Jumla ndogo	52	20	32

